# Ujitokezaji wa Ruwaza ya Shujaa katika Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania

*Felix Kwame Sosoo*
*Chuo Kikuu cha Ghana*
*munguananipenda@yahoo.com*

## Ikisiri

Fasihi imekubaliwa na wataalamu mbalimbali kuwa ni kioo cha jamii kwa kuwa inasawiri yale yaliyomo katika jamii. Kuna wataalamu wengine wanaoona kuwa kwa vile kila jamii ina utamaduni wake, hata kazi zao za fasihi zinatofautiana. Kwa upande mwingine, wapo wataalamu wanaoona kuwa jamii zenye mfanano mkubwa huweza kuwa na kazi za fasihi zinazohusiana. Wataalamu hawa wanaona kwamba, zaidi ya tofauti ndogondogo baina ya jamii hizo, mfanano ni mkubwa kwa kuwa msingi wa falsafa zao unafanana. Kwa mfano, wataalamu hawa huamini kuwa jamii nyingi za Afrika, ikiwamo Tanzania, zaidi ya tofauti ndogondogo miongoni mwao, zina mfanano mkubwa sana. Mfanano huo unaweza kubainika katika masuala mbalimbali kama vile falsafa, matumizi ya motifu mbalimbali, dhana ya ushujaa, mtazamo, fasihi na kadhalika. Hivyo, katika makala haya tunajiuliza, je, kuna mfanano baina ya ushujaa unaosawiriwa na masimulizi ya ngano ya Kiewe na riwaya teule za Shaaban Robert? Je, iwapo mfanano huo upo, unasawiriwaje katika kazi husika za fasihi? Kwa ujumla, makala haya yanakusudia kudadisi jinsi ushujaa unaosawiriwa katika jamii ya Waewe unavyotofautiana na kufanana na ule unasawiriwa katika riwaya teule za Shaaban Robert? Maswali haya yamejenga msingi wa makala haya kwa kutumia kiunzi cha Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa iliyopendekezwa na Campbel (1973); Raglan (1979) na Kunene (1985). Aidha, makala haya yametumia ngano sita za Kiewe kutoka Ghana na riwaya mbili za Shaaban Robert kutoka Tanzania. Katika kazi hizo, mwandishi amechunguza namna ruwaza ya ushujaa inavyosawiriwa katika kumbo hizi mbili, yaani fasihi simulizi ya Waewe na fasihi andishi ya Waswahili.

## 1.0 Utangulizi

Dhana ya fasihi imeelezwa na Nkwera (1979) kuwa ni sanaa itumiayo zaidi maneno na kujishughulisha na jinsi binadamu anavyojitambua mwenyewe binafsi, pia anavyoathiri na kuathiriwa na binadamu wenzake, na viumbe wengine aina kwa aina katika mazingira mbalimbali ya maisha. Njogu na Chimerah (2008) wanaongeza kwa kusema kuwa fasihi ni aina ya sanaa inayotumia lugha ili

kuelezea tajiriba za binadamu. Wanaeleza zaidi kuwa fasihi inaweza kuwa andishi au simulizi, ambapo fasihi andishi huhifadhiwa kimaandishi ilhali fasihi simulizi huhifadhiwa nyoyoni. Pamoja na maoni ya Njogu na Chimerah, fasihi simulizi pia inaweza kuhifadhiwa katika tepurekoda, kanda za CD na njia nyinginezo.

Nkwera *(keshatajwa)*, kwa upande wake anafafanua kuwa fasihi ni moja tu lakini ina njia mbili kuu za uwasilishaji ambazo ni masimulizi ya mdomo na maandishi. Hata hivyo, Ndugo na Wafula (1993) wakinukuliwa na Saleh (2015), wanaeleza tofauti baina ya tanzu hizi mbili kuwa fasihi simulizi ni kongwe wakati fasihi andishi ilikuja wakati wa uvamizi wa wageni wa Kiarabu na Wazungu. Saleh anafafanua kwamba Shaaban Robert na James Mbotela ni miongoni mwa waandishi wa mwanzo wa hadithi ndefu za Kiswahili katika Upwa wa Afrika Mashariki.

Naye, Matteru (1983), anaeleza kuwa fasihi simulizi ndiyo data ya fasihi andishi. Fasihi andishi hutumia fasihi simulizi kuunda maudhui yake. Hata hivyo, maelezo ya wataalamu hawa yanabainisha kuwa kazi za fasihi andishi za awali katika Kiswahili ndizo ambazo ziliegemezwa katika fasihi simulizi, kwani kuna kazi za fasihi andishi ambazo zinajitegemea kabisa. Fasihi simulizi huweza kuwa ni msingi mzuri wa kutoa data itakayotumika kama malighafi ya fasihi andishi. Waandishi wa fasihi ya Kiswahili wananufaika na fasihi simulizi kwa vile huchota miundo na fani mbalimbali za fasihi simulizi na kuzitumia katika kazi zao. Katika kufafanua dhana hiyo, Matteru anawatumia waandishi kama: Shaaban Robert, akitaja vitabu vya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*, kuwa mwandishi ametumia miundo ya kifasihi simulizi. Kwa upande mwingine, Saleh (2015) anawanukuu Mwai na Ndungo (1991) na kueleza kwamba wataalamu hao wameonesha uhusiano baina ya fasihi simulizi na andishi kwa kukubaliana kwamba waandishi wengi wa fasihi andishi wameathiriwa na fasihi simulizi. Kuna wale ambao wameathiriwa kifani na kuna wale ambao wameathiriwa kimaudhui au kwa namna zote mbili. Hata hivyo, wataalamu mbalimbali wa fasihi (taz. Mulokozi, 1996; Wamitila, 2003; Samwel, 2015) wanakubaliana kuwa kila utanzu wa fasihi una sifa za kipekee zinazoutofautisha na utanzu mwingine. Aidha, wengine wanaona kuwa kila utanzu unaweza kuchambuliwa kipwekepweke bila kuuhusisha na mwingine (TUMI, 1988; Okpewho, 1992; Kezilahabi, 1995; Mutembei, 2005). Kwa mujibu wa TUMI (1988) kama walivyonukuliwa na Salim (2015), fasihi simulizi hata ikiandikwa haibadiliki kuwa fasihi andishi. Maelezo ya TUMI yameibua swali miongoni mwa wanazuoni wa fasihi simulizi kuwa, je, fasihi simulizi itasalia kuwa simulizi na fasihi andishi itaendelea kuwa andishi bila kuathiriana hasa kupitia njia za uwasilishaji? TUMI wanaendelea kutetea wazo

lao kwa kusema kwamba kazi simulizi, hata kama ikiandikwa, haibadiliki hadhi, bali huwa imehifadhiwa tu kwa njia hiyo. Pamoja na kwamba tunakubaliana na mawazo ya TUMI na wahakiki wengine kuwa fasihi simulizi hata kama ikiwekwa kwenye maandishi inabaki kuchambuliwa kama fasihi simulizi na fasihi andishi inabaki kuwa fasihi andishi, lakini bado kuna uhusiano mkubwa kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Kupitia uhusiano huo, vipengele vya fasihi simulizi huchotwa na kuingizwa katika fasihi andishi. Kutokana na maelezo haya, makala haya yanakusudia kudhihirisha uhusiano uliopo kati ya fasihi simulizi na andishi, na pia kuonesha uhusiano kati ya fasihi ya Watanzania na fasihi ya Waghana. Ili kulikabili lengo hilo, mwandishi amechambua usawiri wa shujaa unavyojitokeza katika ngano za Kiewe (kutoka Ghana) katika na riwaya za Shaaban Robert (kutoka Tanzania). Aidha, uchambuzi wetu umeongozwa na misingi ya kiunzi cha Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa iliyopendekezwa na Campbel (1973) pamoja na Raglan (1979). Kabla ya kufafanua misingi ya kiunzi cha kinadharia, sehemu ifuatayo inatoa muhtasari wa riwaya teule pamoja na ngano zilizotumika katika makala haya.

## 2.0 Muhtasari wa Kazi Teule za Kifasihi Zilizotumika katika Makala haya

Sehemu hii inabainisha muhtasari wa kazi teule kama zilivyorejelewa katika makala haya.

### 2.1 Muhtasari wa Riwaya Teule

Kama ilivyokwishaelezwa katika utangulizi wa makala haya, mwandishi alikusudia kulinganisha ujitokezaji wa ruwaza ya ushujaa katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* kwa upande mmoja, na ngano za Kiewe kwa upande mwingine.

### 2.1 Muhtasari wa Riwaya Teule (*Kusadikika* na *Adili na Nduguze)*

Riwaya ya *Kusadikika* (1991) inamhusu mhusika anayeitwa Karama. Kama mashujaa wengine wa Kiafrika, Karama anapambana kukomesha ukosefu wa haki katika jamii yake ya Kusadikika, ambayo haikuwa inatoa haki kwa mshtakiwa kujitetea. Hivyo, Karama anapambana kuanzisha elimu ya uanasheria katika nchi yake. Mapambano hayo yanamwingiza Karama katika mvutano na tabaka tawala linalowakilishwa na Majivuno, ambaye alikuwa Waziri Mkuu. Majivuno anamshtaki Karama katika baraza la madiwani. Hata hivyo, kinyume kabisa na utaratibu wa Kusadikika, Karama anaomba ruhusa ya kujitetea mbele ya baraza hilo. Karama anaanza kujitetea kwa kumtumia mjumbe wa Kaskazini aliyeitwa

Burhani. Burhani alikubali kutumwa na Kusadikika kwenda nchi ya Kaskazini licha ya ugumu na umbali wa safari hiyo, Burhani anafungwa kifungo cha maisha.

Mjumbe wa pili anayetumiwa na Karama katika utetezi wake ni Fadhili. Huyu alitumwa Mashariki. Mhusika huyu naye alidharauliwa na kufungwa. Mjumbe mwingine aitwaye Kabuli alitumwa Kusini katika utetezi huu. Hata hivyo, Karama anaeleza kwamba huyu naye aliporudi na kueleza aliyoyaona huko ili kuistawisha jamii ya Kusadikika, alikataliwa na kutupwa gerezani kwa kifungo cha maisha na kazi ngumu. Karama anaendeleza utetezi wake ambapo anamtumia pia mhusika Auni, mjumbe wa Magharibi. Mawazo ya Auni hayakukubaliwa isipokuwa aliadhibiwa kama watangulizi wake. Utetezi uliofuata ulimhusisha Ridhaa, mjumbe aliyetumwa Mbinguni. Naye, anaadhibiwa kama waliomtangulia bila hata kupongezwa.

Utetezi mwingine wa Karama ulikuwa unamhusu mjumbe wa Ardhini. Huyu alijulikana kama Amini. Naye anaadhibiwa kwa kunyang'anywa madaraka. Kwa kifupi, Shaaban Robert katika kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji, anatumia sifa, kaida na tabia mbalimbali za zinazoakisi ruwaza mbalimbali za motifu ya safari za mashujaa. Miongoni mwa ruwaza hizo ni safari, motifu ya msako, ujasiri, uhodari, na kujitoa kwa ajili ya jamii. Sifa hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuwajenga wahusika wa riwaya ya *Kusadikika* kiasi cha kuonekana kama mashujaa wengine wanaosawiriwa katika kazi na tanzu zingine za kifasihi, hususani ngano.

Riwaya nyingine iliyotumika katika makala haya ni ya *Adili na Nduguze* (2010). Riwaya hii inamhusu Adili na ndugu zake waliokuwa chini ya utawala wa Mfalme Rai wa Ughaibu. Pato kuu la nchi ya Ughaibu ni kodi itokanayo na wanyama. Watu wake wana bidii katika kazi. Kodi inapatikana katika miji mikubwa miwili ambayo ni Ughaibu na Janibu lakini baadaye Mfalme Rai anagundua kuwa kodi inapungua kwa kuwa raia wa Janibu hawatoi kodi ambako Adili alikuwa anaishi. Mfalme anamtuma mjumbe kwenda Janibu kutafiti ni kwa nini hawapeleki mapato. Mjumbe anagundua kuwa mapato ya Janibu yameongezeka, hivyo, muda wa ukusanyaji pia umeongezeka. Baada ya kukamilisha ukusanyaji, mjumbe anapatiwa mapato na kurudisha kwa Mfalme. Hata hivyo, anagundua siri nyingine ya adhabu ya manyani inayoendelea nyumbani kwa Adili. Jambo hili linamsikitisha sana Mjumbe na anaamua kutoa siri kwa Mfalme. Mfalme anaamuru Adili na manyani wafikishwe Ughaibu kwa Mfalme.

Mwandishi anaelezea namna manyani yanavyofikishwa kwa Mfalme na

kuonesha hali ya kutaka msaada kwa mateso wanayopata. Adili anaamriwa kusimulia ukweli kuhusu maisha ya manyani. Mwandishi anatumia mbinu mbaimbali za kisanaa kusawiri matukio mbalimbali ndani ya riwaya yake. Inasimuliwa kuwa kulikuwa na mji mmoja ambao watu wake wote waligeuzwa kuwa mawe. Kutokana na safari zake, kwa vile kila binadamu aliyekuwako katika mji huo aligeuka jiwe, Adili anafaidika na mji huu kwa kupata vitu vya thamani lakini hawezi kuvisafirisha.

Mwandishi anaendelea kueleza kuhusu kutoswa kwa Adili. Adili anatoswa na nduguze baharini baada ya kuwaletea mali nyingi na mwanamke mrembo ambaye anakuwa chaguo la Adili lakini nduguze wanamwonea wivu na wanataka awe mke wa wote. Adili anapokataa, nduguze wanamfunga na kumtosa baharini. Adili anarudishwa chomboni kuendelea na safari akiongozana na Huria. Huria ni jini anayewapa nduguze adhabu ya kumtosa Adili baharini. Wanageuzwa manyani na kuahidiwa adhabu kali ya viboko hadi kuzimia kila siku usiku wa manane baada ya kufika Janibu.

Kwa ufupi, katika riwaya ya *Adili na Nduguze,* mwandishi Shaaban Robert anaonesha ujuzi wake katika kusawiri motifu mbalimbali za ushujaa. Wahusika waliomo ndani ya riwaya hii wanaakisi hali halisi ya motifu zinazoambatana na ruwaza ya shujaa ikiwa ni pamoja na motifu ya safari na motifu msako. Kutokana na motifu hizo, wahusika wanasafiri kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine. Kama ilivyo kwa riwaya ya *Kusadikika*, riwaya ya *Adili na Nduguze* inasawiri ruwaza ya shujaa na ushujaa kwa namna ya kipekee kiasi cha kufanana mno na ruwaza za mashujaa wanaosawiriwa katika fasihi simulizi ya jamii mbalimbali duniani, ikiwamo jamii ya Waewe, nchini Ghana.

## 2.2 Muhtasari wa Ngano za Kiewe na Waewe

Ili tuweze kujadili na kuzungumzia ngano za Waewe, ni vyema pia tuzungumze kuhusu eneo ambalo ngano hizi zinatokea. Ni vyema tujue historia fupi na eneo la kijiografia la Waewe ili kurahisisha uelewa wa ngano zao. Waewe ni kundi la jamii katika Afrika. Ni kundi au jamii kubwa zaidi nchini Togo linalowakilisha asilimia 32 ya raia wote, na pia jamii ya tatu kubwa zaidi nchini Ghana.[1] Waewe pia ni miongoni mwa jamii zinazoishi nchini Benin, Ivory Coast na Nigeria. Wanaongea lugha ya Kiewe ambayo ni miongoni mwa lugha za Niger-Congo.[2]

1 Taz. https://www.cia.gov/library/publications/the-world-factbook/geos/gh.html

2 Taz. http https://www.ethnologue.com/language/ewe

Vilevile, Waewe pia wana uhusiano na watu wanaoongea lugha iitwayo *Gbe*[3] kama *Fon, Gen, Phla Phera* na watu wa *Aja* kutoka Togo na Benin. Hata hivyo, miaka mingi iliyopita, kuna wanahistoria waliowahusisha Waewe na jamii ya Wa-Akan na Wayoruba lakini tafiti nyingi zilizofanyika baadaye zilionesha kuwa jamii ya Waewe ni tofauti kabisa na jamii hizo.

Kama ilivyo kwa jamii nyingine nyingi za Kiafrika, Waewe walikuwa na uhusiano na wakoloni na wafanyabiashara kutoka Ulaya kabla ya kuanza kwa vita baina yao na Wadachi. Walipambana na Wadachi mwaka 1784 wakati Wadachi walipotaka kujenga ngome pwani mwa eneo lao kwa ajili ya shughuli za kiutawala na biashara. Waewe wana falme mbalimbali zinazojitegemea ambazo huishi katika Jamhuri ya Togo na Kusini Mashariki mwa Ghana, na hasa katika mkoa wa Volta (Nukunya, 1969).

Wataalamu mbalimbali wanatoa fasili ya ngano za jamii tofautitofauti. Kwa mujibu wa Dzakpasu (1981), istilahi ya *folktales* yaani ngano ilitumika kwa mara ya kwanza na Wiliam Thomas mnamo mwaka 1846. Mtaalamu huyu aliitumia dhana hii kumaanisha mambo ya kale ya Waingereza wa vijijini. Maelezo haya yanaonekana kuungwa mkono na Nkwera (1979) anayesema kuwa ngano ni hadithi za kale zielezazo mambo ya zamani yaliyosadikiwa na taifa au kabila fulani. Anaendelea kusema kuwa yaweza kuwa mambo ya kweli au ya kubuni tu, ama yote kwa pamoja pasipo kutofautiana.

Naye, Sidahome (1964) anasema kuwa ngano ni muunganiko pekee baina ya watu na tamaduni zao. Hoja ya Sidahome inadokeza kuwa ngano kwa Waafrika ni zaidi ya kuangaliwa kwa jicho la kisimulizi tu bali ni muunganiko baina ya wakati wa sasa na wakati wa zamani. Hii inamaanisha kuwa uhusiano wowote mwingine ambao Waafrika wanao na wakati wao wa zamani, tofauti na zilizoandikwa, ni kupitia njia ya masimulizi ndipo mawazo na tamaduni zao zinaweza kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Makala haya yametumia ngano kulinganisha ruwaza ya shujaa na ushujaa katika jamii za Watanzania na Waghana.

Ngano ambayo inaitwa *Gli* katika lugha ya Kiewe ni hadithi inayosimulia masuala yanayowakilisha tamaduni na maisha ya jamii hiyo. Kumbo hii ya fasihi simulizi inatumika kuelimisha jamii ambayo inakuwa katika mfumo wa kuchanganya maadili, mafunzo na starehe kwa pamoja. Vilevile, *Gli* inatumia mbinu ya kuchukia tabia mbaya, ambayo haikubaliki katika jamii na kuhimiza

3 Hii ni lahaja ya Kiewe inayozungumzwa na watu wa Benin na Togo.

tabia zinazokubalika katika jamii. Aidha, kwa kutia moyo wanajamii wa Kiewe, ngano nyingi zinazosimuliwa zinawekwa katika mitindo mbalimbali. Mfano, wa mtindo unaotumiwa na fanani ni kuwajenga wahusika wake katika motifu ya safari, msako na motifu mbalimbali.

Akizungumzia kuhusu ngano za Waewe, Dzakpasu (1981) anasema kuwa ngano ni usimulizi wa mdomo, hivyo, si rahisi kupata sifa zake za kifasihi mpaka itendeke na kuchambuliwa kama ilivyosimuliwa au ilivyotiririshwa kutoka kizazi hadi kizazi. Aidha, ni muhimu kuzingatia sifa zinazoyafanya masimulizi kuwa fasihi au kazi ya sanaa. Hii inamaanisha kuwa kuhusisha usimulizi wa ngano na fasihi haimaanishi kuwa kila masimulizi ya Waewe ni ngano. Hivyo, ni muhimu kusisitiza kuwa siyo kila ngano za Kiewe zinabeba sifa za fasihi. Kuna baadhi ya fanani wanaofurahia utungaji na usimulizi wa ngano kwa kuzingatia sifa maalumu zinazoifanya kuwa ngano. Kwa mujibu wa Whorf (1956), fanani anatakiwa kuzingatia sifa maalumu zilizopo katika lugha husika, au jamii kwa kutunga ngano. Anaendelea kusema kuwa fanani wanapaswa kuhakikisha kuwa masimulizi yanaendana na mfumo wa lugha inayotumika, sarufi na sifa nyingine wakitiririsha uhalisia na maana ya masimulizi haya. Katika jamii ya Waewe kila mtu ana uwezo wa kusimulia ngano, lakini si kila mtu anaruhusiwa kusimulia ngano. Lengo letu katika makala hii si kuzungumzia suala la ni nani anahusika katika usimulizi wa ngano. Hivyo, kwa kuzingatia maelezo na usuli huu wa maisha, historia na fasii simulizi ya Waewe, makala haya yametumia ngano teule sita za Kiewe. Ngano hizo zimeteuliwa kwa kuwa zimesheheni masuala muhimu yanayoakisi ruwaza ya shujaa ikiwa ni pamoja na motifu za safari na msako.

## 3.0 Kiunzi cha Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa

Kama ilivyokwishaelezwa hapo awali kwenye utangulizi wa makala haya, ili kuyafikia malengo ya uchambuzi wetu, tumeongozwa na misingi ya kiunzi cha Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa iliyopendekezwa na Campbel (1973) pamoja na Raglan (1979). Kwa mujibu wa Campbel (1973), ruwaza ya shujaa imejengwa na hatua kuu tatu ambazo ni: (i) shujaa kuondoka; (ii) kukutana na vikwazo na kuvishinda, na (iii) kurudi katika jamii na kupigana na kupata ushindi. Aidha, Brown (1990) anathibitisha wazo la Campbel kwa kusema kuwa katika hatua ya kwanza shujaa anasafiri na kwenda nchi za mbali. Katika hatua hii ya kwanza,

shujaa bado hajakomaa wala hajawa mbobevu wa kupambana na matatizo au changamoto mbalimbali. Katika kusisitiza umuhimu wa hatua hii ya kuondoka kwa shujaa, Nyamsenda (2015) anawanukuu Propp (1958), Campbel (1973), Raglan (1979) na Kunene (1985) na kuelezea kwamba miundo au ruwaza ya safari ya shujaaa hutegemea chanzo cha safari yenyewe. Kwa hivyo, safari ya shujaa yaweza kujitokeza katika namna tatu:

(i) Shujaa anapoondoka na kukusudia kurudi nyumbani.
(ii) Shujaa anapoondoka na hakusudii kurudi nyumbani.
(iii) Shujaa anapoondoka, anakusudia kurudi, lakini kuna kikwazo kinachomzuia asirudi nyumbani.

Katika hatua ya pili shujaa anakutana na vikwazo, misukosuko na majaribu ambayo yanamfunda na kumkomaza. Katika hatua hii, shujaa huwa anapata ukomavu wa kifikra zaidi na kupata ujasiri zaidi kuliko aliokuwa nao katika hatua ya awali. Ukomavu huo ndio unaomwezesha kuvishinda vikwazo mbalimbali. Hatua ya tatu, shujaa anarejea kwao, na ni katika hatua hii ambapo maazimio ya shujaa hudhihirika. Anapofika kwao, shujaa hukaribishwa na kupata hadhi na heshima kubwa na hatimaye kuwa mtawala.

Kwa upande mwingine, Kunene (1985) ameelezea nadharia hii katika kufafanua motifu ya safari za shujaa. Yeye anaangalia safari ya shujaa kwa namna mbili yaani safari ya nje na safari ya ndani au ya kisaikolojia. Safari ya nje inahusisha mwenendo wa kutoka sehemu moja hadi nyingine wakati safari ya ndani ni masafa mafupi. Kwa mujibu wa Senkoro (1997), kitendo cha shujaa kuondoka mahali alipozaliwa na kwenda ugenini huwa ni cha muda mfupi zaidi. Kitendo hicho kinarejelea safari ya nje. Kwa upande mwingine, safari ya ndani hurejelea safari ya shujaa anapopitia hatua mbalimbali za ukuaji kutoka utotoni hadi ukubwani. Jambo hilo linasawiriwa kisaikilojia zaidi.

Kadhalika, Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa imeelezwa na Raglan (1979). Kwa mujibu wa Raglan, ruwaza au mikondo ya safari za shujaa imeundwa na hatua ishirini na mbili. Hatua hizo humtokea shujaa wa tamaduni zote duniani. Kimsingi, Raglan (1979) alitumia ruwaza hizi ishirini na mbili kueleza namna usawiri wa ruwaza za mashujaa unavyojitokeza katika jamii na tamaduni mbalimbali ulimwenguni. Baadhi ya ruwaza hizi ni kwamba, Mama wa shujaa ni binti mfalme bikira, Baba yake ni mfalme (tabaka la juu), mara nyingi ni ndugu wa karibu wa mama yake, lakini mazingira ya kuzaliwa kwa shujaa si ya kawaida, shujaa

anasadikika kuwa mwana wa Mungu, Anapozaliwa linafanywa jaribio aghalabu na baba yake la kumuua, lakini, anatoroshwa kwa siri (kwa kutaja kwa uchache).

Pamoja na mambo mengine, mchango mkuu wa Raglan katika kuiendeleza nadharia hii umedhihirika hasa kupitia maelezo yake kuhusu nafasi ya mwanamke katika kusawiri motifu za ushujaa. Hii ina maana kwamba, Raglan amechangia kwa kuonesha usawiri wa shujaa mwanamke katika fasihi na jinsi mwanamke anavyochangia kujitokeza kwa mashujaa wengine katika jamii. Raglan amethubutu kubainisha sifa za mashujaa wa kike na jinsi sifa hizi zinavyofanana na sifa za mashujaa wa kiume. Anawataja baadhi ya mashujaa wa kike/wanawake kama Leia/Malikia Leah (nyota wa vita), Guinivere, Tori Amos, Cleopatra VII, (kwa kuwataja wachache).

Aidha, mtazamo wa Raglan kuhusu shujaa mwanamke na mwanaume unaendelezwa pia na Johnson (2008, 2009). Johnson amefasili dhana ya shujaa na ushujaa na kutokana na fasili hiyo ametoa mifano ya mashujaa wanaume na wanawake kutoka miktadha mbalimbali ya fasihi. Hatimaye, mtaalamu huyu anatoa rai kwa wale wanaodhani kwamba dunia hii haina mashujaa kabisa waweze kusoma katika uga huu ili wapate maarifa. Anaonesha mashujaa kuanzia kwa Alexander the Great na Julius Caesar mpaka kwa Churchill na de Gaulle; na wengine anaowaeleza ni pamoja na Samsoni, Lady Jane Grey, Malikia Mary wa Scots, Charles de Gaullle na Margaret Thatcher Judith na wengine wengi.

Kwa ujumla, mawazo ya wataalamu waliotajwa katika sehemu hii kuhusu Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa yanataja na kubainisha misingi mahususi mwafaka katika kupambanua ruwaza ya wahusika mashujaa katika fasihi. Misingi hiyo imeegemea katika masuala matatu ambayo ni: (i) dhana ya ushujaa; (ii) sifa za shujaa; na (iii) motifu zinazombana na ruwaza ya shujaa. Sehemu ifuatayo imefafanua kwa kina misingi hii:

### 3.1 Dhana ya Ushujaa

Kwa mujibu wa TUKI (2004), ushujaa ni hali ya moyo thabiti, uhodari, ujasiri, ushakii na hamidha. Kwa mujibu wa Robert (1991), ushujaa kwa mtu ni ngao, kwa nchi ni tegemeo na kwa taifa ni uwezo. Aidha, Robert *(keshatajwa)* anafafanua kuwa kuna namna mbili za ushujaa ambazo ni ushujaa wa nguvu na silaha na ushujaa wa ukweli na nasaha. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa, ushujaa ni jitihada ya kuwatumikia na kuwaokoa wengine wote kwa namna yoyote na siyo jitihada ya kuwashinda wengine wote kwa namna yoyote. Katika jamii

mbalimbali mashujaa wengi, hujitoa kuwasaidia wengine. Ushujaa unajidhihirisha kwa mtu au kundi la watu wanaofanya jambo kwa niaba ya wengine kwa kusudi la kuleta furaha, maendeleo, kulinda heshima ya jamii au kuleta amani katika jamii. Aidha, Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa inasisitiza kuwa kila jamii ina namna yake ya kuelezea maana ya shujaa, lakini kimuundo mashujaa wote wana sifa na mienendo inayoshabiana. Hivyo, namna nzuri ya kueleza ujitokezaji wa ruwaza ya shujaa katika fasihi ni kuchunguza na kuona mtazamo wa jamii kuhusu dhana nzima ya shujaa. Katika makala haya, tumetumia msingi huu kutazama jinsi jamii ya Waewe inavyomsawiri shujaa, na jinsi jamii ya Watanzania kupitia riwaya za Shaaban Robert inavyomsawiri shujaa. Suala hili limefafanuliwa vyema kwa kurejelea tofauti ya usawiri wa ruwaza ya shujaa katika jamii zote mbili.

### 3.2 Sifa za Shujaa

Ingawa, Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa inatambua kuwa kila jamii ina mtazamo wake kuhusu maana na dhana ya shujaa, wataalamu mbalimbali wanaona kuwa sifa za shujaa zinafanana na kuelekeana katika jamii mbalimbali duniani. Mulokozi (1999) akiongelea ushujaa katika jamii ya Wahaya, anasema shujaa wa Kihaya ana silaha au sifa mbili. Anazitaja sifa hizi kama uwezo wa kimwili, kiakili pamoja na nguvu za sihiri. Mulokozi *(keshatajwa)* anaendelea kusema kuwa uwezo wa kudhibiti nguvu za sihiri unahusisha maarifa ya ndani ambayo lazima yawe siri. Akifafanua zaidi, Mulokozi (2012) anasema shujaa hushiriki katika safari ya mzunguko (dawari) ya msako, hupambana na wapinzani ambao hujaribu kumzuia kuendelea na safari yake na hurejea nyumbani akiwa amebadilishwa sana na safari yake hiyo.

Kwa ufupi, kutokana na msingi huu wa sifa za shujaa tunatambua kuwa shujaa ni mtu mwenye kujipamba kwa sifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na nguvu za kimwili na wakati mwingine kisihiri, shujaa huwa na ujasiri na uhodari na kutokana na hayo, hujiamini na hawi mwoga. Hivyo, katika makala haya, wahusika wanaofikiriwa kuwa ni mashujaa wamebainishwa kwa kurejelea sifa walizokuwa nazo.

### 3.3 Motifu

Msingi mwingine wa Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa ni motifu. Kwa mujibu wa Thompson (1932) akinukuliwa na Dorson (1972) motifu ni kipengele radidi kipatikanacho katika sanaa jadiya; ni maelezo ambayo masimulizi yote

yanajinasibisha nayo. Anaendelea kueleza kuwa motifu ni kipengele ambacho kinaweza kujikita ndani ya masimulizi, ndani ya matendo yaliyo katika masimulizi na mara nyingine katika hali inayojitokeza sana katika tendo lililo ndani ya usimulizi. Kimsingi, ingawa kinadharia, motifu inajihusisha zaidi na vipengele vya kimaudhui, lakini kiutendaji motifu inaelekea kuwapo katika maudhui na fani. Wazo kuwa motifu ni kipengele kinachoweza kupatikana katika maudhui na fani ya kazi za kifasihi linawekwa bayana zaidi na Mulokozi (1996) anaposema kuwa motifu ni kipengele radidi cha kijadi/kikaida cha kifani au kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Wazo la Mulokozi linashabihiana kwa namna fulani na wazo la Tavris (1998) anayeeleza kuwa motifu ni dhana au wazo linalojitokeza kuanzia mwanzo wa hadithi, au kazi yoyote ya fasihi hadi mwisho wa kazi hiyo na hata katika kazi nyingine ili kujenga ruwaza fulani. Anaendelea kusema kuwa motifu ni picha, ishara au dhamira zinazojirudiarudia katika kazi moja ya fasihi au hata nje ya kazi hiyo.

Maelezo haya yanathibitisha kuwa motifu ni msingi imara wa Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa unaotumika katika kupambanulia ruwaza, miundo na hali za wahusika mashujaa katika fasihi simulizi na fasihi andishi. Hivyo, motifu inaweza kujikita kwa mhusika fulani ndani ya masimulizi kimatendo na katika hali inayojirudiarudia katika tendo lililo ndani ya utambaji au usimulizi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), dhana ya motifu hutumiwa kurejelea wazo kuu na sehemu ya dhamira katika kazi ya kifasihi. Huweza pia kuelezea elementi ya kimaudhui au kifani inayotawala kazi fulani. Pia, Mwangoka (2011) anasema kuwa umuhimu wa motifu anaouelezea Wamitila *(keshatajwa)* kwa kuzingatia maudhui na fani unamaanisha kwamba, kuwapo kwa motifu za namna mbalimbali katika hadithi ndiko kunakobeba muundo na maana ya hadithi. Kutokana na maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu motifu, tunaweza kufafanua kuwa motifu ni kipashio muhimu kinachoweza kutumika kuonesha ujitokezaji wa ruwaza ya shujaa katika kazi za kifasihi. Katika makala haya tumeongozwa na mtazamo huu kwa kujikita kwenye motifu kuu mbili zinazojitokeza kwa pamoja (motifu za msako na safari), na hivyo tukafanikiwa kuonesha jinsi ruwaza ya shujaa inavyojitokeza kupitia motifu ya safari ya msako. Kwa namna ya kipekee, tumebaini kuwa motifu imetumika kuonesha picha, sauti au matendo ya wahusika, safari zao, matumaini yao na majaribu waliyokutana nayo katika safari hizo. Motifu kama msingi wa Nadharua ya Ruwaza ya Shujaa imesaidia siyo tu kupambanua ruwaza za shujaa katika ngano na riwaya zilizochambuliwa bali pia imetusaidia kuona tofauti na

mshabaha uliopo kati ya ujitokezaji wa ruwaza hizo nchini Ghana na Tanzania. Katika sehemu ifuatayo, tumechambua kwa kina kufanana na kutofautiana kwa ujitokezaji wa ruwaza ya shujaa kwenye ngano za Kiewe kutoka Ghana na riwaya teule kutoka Tanzania.

## 4.0 Ujitokezaji wa Ruwaza ya Ushujaa Katika Ngano za Kiewe na Riwaya Teule

Katika kuonesha jinsi ruwaza ya shujaa inavyojitokeza kwenye ngano za Kiewe na riwaya za Shaaban Robert, mwandishi amefanikiwa kubaini kuwa ujitokezaji huo unaakisi kufanana na kutofautiana kati ya fasihi simulizi ya Ghana (jamii ya Waewe) na jamii ya Watanzania (fasihi ya Kiswahili).

### 4.1 Mfanano Baina ya Ngano za Kiewe na Riwaya Teule za Shaaban Robert

Makala haya yamebaini kuwa kuna mfanano mkubwa baina ya ngano teule za Kiewe na riwaya teule za Shaaban Robert katika namna ya kusawiri ujitokezaji wa ruwaza ya shujaa na dhana ya ushujaa. Aidha, katika sehemu zote mbili ruwaza ya shujaa na dhana ya shujaa zimepambanuliwa kupitia nyenzo kuu ya Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa: motifu ya safari ya msako. Kutokana na mtazamo huo, ujitokezaji wa ruwaza na dhana ya shujaa vimejitokeza katika hatua tatu za kuondoka, majaribu na kurejea kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Mfanano Katika Kuondoka kwa Shujaa

Kipengele cha kwanza kinachoonesha kufanana kwa ujitokezaji wa ruwaza na dhana ya shujaa kati ya zilizochambuliwa ni katika ruwaza ya kuondoka kwa shujaa. Jambo hili limesawiriwa kwa namna mbalimbali katika ngano na katika riwaya teule. Katika ngano iitwayo *Asiyesikia la Mkuu, Huvunjika Guu,* fanani anatuambia kuhusu mhusika Atsu ambaye anaondoka na kwenda kwenye safari ya kutafuta filimbi yao waliyoisahau shambani kwa bahati mbaya. Msimulizi anasimulia namna Atsu alivyotembea kwa kupita katika misitu mikubwamikubwa huku akitafuta filimbi hiyo. Atsu alionesha ushujaa wake pale anapoweka pembeni ushauri wa dada yake na wazazi wake. Alikataliwa kwenda shambani muda ule wa usiku kwa ajili ya kutafuta filimbi. Hali kama hii inabainika pia katika ngano ya *Umoja ni Nguvu*. Katika simulizi hiyo, tunaona wahusika farasi, mbwa, jogoo na paka wanaondoka na kusafiri kutoka vijijini kwao kutafuta sehemu yenye

amani na utulivu ambapo hawatauawa na mtu yoyote. Hali hii imedhihirishwa pale fanani anaposema:

> Farasi alisikia kila kitu na hivyo akaamua kutoroka alfajiri na kwenda sehemu ya mbali ili afe kifo cha kawaida kuliko kuuwawa na mtu.

Vilevile, katika ngano ya *Kuwornu na Watoto Wake*, Mawusi anaondoka kutoka kwa kaka yake kutokana na kufanyiwa mambo mengi mabaya.

Ruwaza ya kuondoka kwa shujaa kama inavyosawiriwa katika ngano za Kiewe pia imejitokeza katika riwaya teule. Katika riwaya ya *Kusadikika,* mwandishi anazungumzia kisa cha wajumbe sita waliosafiri kwenda nchi mbalimbali kutafuta masuala mbalimbali yenye tija kwa taifa lao la Kusadikika. Aidha, mwandishi anasimulia ushujaa wa Karama ambaye ingawa hajasafiri lakini anatumia visa vya wahusika wengine waliosafiri kama ushahidi na utetezi wake. Katika riwaya hii motifu ya safari siyo tu kuwa ni kichocheo cha wahusika kuondoka bali pia ni kichocheo cha wahusika kutetea masilahi yao binafsi na masilahi ya wengine. Ndiyo maana Karama katika utetezi wake wa kuanzisha elimu ya sheria anazirejelea safari za wajumbe sita ambao walionesha ushujaa wao kupitia vikwazo mbalimbali walivyoshinda kwenye safari zao. Safari za kuondoka kwa wajumbe hao, kama zilivyokuwa safari za wahusika wa ngano, zilikusudiwa kutatua tatizo lililopo katika jamii wanazoishi na pia zilikuwa na changamoto nyingi. Miongoni wa wajumbe hao sita walioondoka ni pamoja na Buruhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Amini na Ridhaa. Wajumbe hawa wote walisafiri kwenda nchi mbalimbali kutafuta maendeleo ya nchi ya *Kusadikika.* Mhusika mwingine katika riwaya teule aliyeondoka anabainika katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Katika riwaya hii mwandishi anasimulia kuhusu safari ya Adili na ndugu zake wanaposafiri kutoka nchi yao ya Janibu kwenda nchi nyingine kwa ajili ya kufanya biashara.

### 4.1.2 Mfanano katika Hatua ya Shujaa Kukutana na Majaribu

Kadhalika, mwandishi amebaini kuwa ruwaza nyingine iliyotumika kusawiri ushujaa wa wahusika ni kupambana na changamoto au vikwazo. Jambo hili limeonekana kuwa na mshabaha mkubwa kati ya ngano za Kiewe na riwaya teule. Katika kazi zote hizi za kifasihi, wahusika mashujaa walisafiri na katika safari zao walikutana na majaribu au vikwazo mbalimbali. Jambo hili linaonesha kuwa

ushujaa wa wahusika unadhihirika kupitia juhudi zao za kupambana na vikwazo hivyo. Motifu za msako, safari na safari ya msako zinazoonekana katika kazi hizi zinamtaka shujaa aoneshe ushupavu wake katika kukabiliana na misukosuko au majaribu yanayomkabili. Hivyo, ushujaa wa wahusika unabainika kutokana na uwezo wake katika kupambana na vikwazo mbalimbali anavyokumbana navyo. Katika kupambana na kujitokeza mshindi, anajitofautisha na watu wengine katika jamii. Utofauti huu ndio unamfanya shujaa atambulike katika jamii yake kama shujaa.

Katika ngano ya *Kuwornu na Watoto wake*, tunaona jinsi shujaa Mawusi alivyopata tabu baada ya kufa kwa wazazi wake. Bila shaka ushujaa wake ulitokana na uwezo wake wa kuvumilia shida na misukosuko hiyo. Kadhalika, Mwandishi Shaaban Robert anasawiri ushujaa wa wahusika kupitia ruwaza ya shujaa kukutana na misukosuko katika riwaya zake kama ilivyo katika ngano za Kiewe. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kusadikika,* Buruhani, mjumbe wa mwanzo aliyeenda nchi ya Kaskazini, Kabuli naye alikwenda nchi ya Kusini, Auni alikwenda nchi ya Magharibi, Amini aliyekwenda nchi ya Ardhini, Fadhili aliyekwenda nchi ya Mashariki na Ridhaa mjumbe wa mwisho aliyekwenda nchi ya Mbinguni; wote walikutana na vikwazo vingi lakini walipambana navyo mpaka wakavishinda na kurudi kuwa mashujaa.

Katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, shujaa Adili katika safari yake aliyotoka kwenda kufanya biashara na ndugu zake, alikutana na vikwazo na majaribu mbalimbali. Mwandishi anatuambia kuwa baada ya kutia nanga meli yao kwa ajili ya kwenda kutafuta maji ya kunywa, Adili aliona mji, kwa hiyo, akaenda katika mjio huo ili apate maji ya kunywa. Kwa bahati mbaya katika mji ule kila kitu kilikuwa ni mawe, mavumbi na michanga, hivyo, hakukuwa na dalili ya maji. Ili kushinda jaribu hili Adili alikwenda mbali zaidi ndani ya mji huo na akafanikiwa kupata komamanga ambalo lilitosha kuwaondolea kiu mabaharia wote jahazini. Kikwazo kingine ambacho Adili alikumbana nacho ni wivu wa ndugu zake. Kutokana na wivu huo ndugu zake walimtosa baharini. Aidha, Adili alitoswa baharini kwa kuwa ndugu zake walimtamani mwanamke ambaye Adili alikuja naye kutoka mji wa mawe. Kikwazo kingine kwa Adili kilitokea pale Adili anapopigwa kwa kukosa kuwaadhibu ndugu zake. Pamoja na majaribu yote hayo Adili anaibuka kuwa mshindi kwa kuwa anavumilia na hakati tamaa.

Kutokana na uchambuzi uliofanyika, tumegundua kuwa mashujaa wengi katika ngano za Kiewe na riwaya teule wanakumbana na vikwazo ambavyo wanashinda

ili kufanikisha safari yao. Suala hili linajitokeza katika jamii nyingine ya Kiafrika. Kwa mfano, Nyamsenda (2015) anapozungumzia sifa za shujaa miongoni mwa jamii ya Waikizu na kusema, "Ushujaa sisi Waikizu tunautafsiri kwamba ni kitendo cha kupambana na mambo magumu na mazito na kuyashinda, huu ndiyo ushujaa. Hivyo basi, hatutegemei kuona kikwazo kinamzuia shujaa kurudi nyumbani, huu ndio utamaduni wetu na jadi yetu tangu zamani."

### 4.1.3 Mfanano katika Kurudi kwa Shujaa

Mbali na kufanana katika msukumo wa safari, na kukutana na misukosuko kwa shujaa, uchambuzi wetu pia umebaini kuwa kazi zilizochambuliwa zinaonesha kuwa ruwaza ya shujaa inajitokeza kwa namna ileile katika kipengele cha kurejea kwa mashujaa kutoka safarini. Wataalamu mbalimbali wanabainisha kwamba shujaa anaposafiri lazima arudi kutoka kwenye safari yake ili kuleta mabadiliko katika jamii yake. Akifafanua hili, Nyamsenda (2015) anasema kuwa katika jamii ya Waikizu kama shujaa hatarajii kurudi nyumbani, basi huyo si shujaa. Kwa sababu ushujaa wa shujaa hudhihirika kupitia kurejea kwake katika maskani yake ya asili hata motifu za safari ya msako zinazosawiriwa kwenye ngano zna riwaya zilizochambuliwa nazo zinaonesha jambo hilo. Hivyo, tathmini ya mwisho kwa jamii hizi ikiwa mhusika ni shujaa au siyo shujaa ni kutazama ikiwa atarudi au hatarudi.

Katika makala haya imebainika kuwa wapo mashujaa ambao wanarudi lakini pia wapo mashujaa ambao hawarudi. Katika jamii ya Waewe, siyo lazima shujaa arejee nyumbani. Pamoja na sababu mbalimbali za kwa nini shujaa anasafari, shujaa katika jamii ya Waewe hutoka kwao kwa sababu mbalimbali kama kutafuta usalama wake au kukimbia ili asiuawe. Vilevile, kuna aina nyingine za safari ambazo shujaa hawezi kurejea alikotoka.

Katika ngano za Kiewe na riwaya teule tunaona kwamba ingawa shujaa anakumbana na matatizo mengi sana njiani lakini anapambana nayo na kuyashinda kwa namna ya pekee sana na hatimaye shujaa hufanikiwa kurudi nyumbani. Kwa mujibu wa Kiango (1974), mara zote shujaa anayehusishwa na motifu ya safari hupambana na vikwazo kwa minajili ya kujinufaisha yeye mwenyewe binafsi na si kwa manufaa ya jamii yake. Hata hivyo, katika makala haya, tumebaini kuwa shujaa husafiri siyo kwa manufaa yake binafsi pekee bali pia kwa manufaa ya jamii yake. Uchambuzi wetu unaonesha kuwa sababu ya shujaa katika jamii ya Waewe na kama inavyojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika* ni kusaidia nchi

yake katika kutatua shida za jamii zao. Kwa mfano, katika ngano ya *Mapacha na Bibi Kizee,* tunasimuliwa kuhusu mapacha wawili Atsu na Etsey. Wakati kulipokuwa na njaa katika jamii, mapacha hawa wawili walisafiri ili waweza kuleta chakula nyumbani kwa familia zao. Vilevile, tunasimuliwa kuwa Atsu alirudi na ngoma ambayo alipoipiga na kutamka, chakula kilitokea. Kilipotokea chakula hicho kiliwatosha watu wote. Suala hili linadokeza kuwa kurejea kwa wahusika kunawafanya wajulikane au watambulike katika jamii kuwa wao walikuwa na shabaha gani katika maisha yao.

Kama ilivyo katika jamii ya Waewe, mwandishi Shaaban Robert pia katika riwaya ya *Kusadikika* anasimulia kuwa safari za mashujaa ni za msako na zinafanywa kwa minajili ya kuinufaisha jamii nzima. Katika riwaya hii, mwandishi anatuambia kuhusu safari ya wajumbe sita waliosafiri kwenda nchi mbalimbali ili waweze kuleta mambo mema kwa jamii yao. Katika kuonesha mfanano wa suala hili, ni dhahiri kuwa kila mjumbe aliyesafiri alirejea katika nchi yake ya Kusadikika. Hii inaonyesha mfanano mkubwa uliopo katika jamii ya Waewe na Waswahili.

### 4.1.4 Kauli ya Jumla kuhusu Kufanana kwa Ujitokezaji wa Ruwaza ya Shujaa

Katika sehemu iliyopita tumeonesha jinsi ruwaza ya shujaa inavyosawiriwa kwenye ngano na riwaya teule. Kimsingi, imeonshwa waziwazi kuwa ruwaza hizo hujidhhirisha kupitia miundo mikuu mitatu ya safari za mashujaa: kuondoka, majaribu na kurejea. Hata hivyo, jambo kubwa la kuzingatia hapa ni kuwa ingawa ruwaza ya shujaa kwa kiwango kikubwa imesawiriwa kupitia muundo wa motifu ya safari ya msako, siyo lazima safari za wahusika ziwe ni za kuonekana. Wakati mwingine kuna safari za ndani ambazo ni kufikirika tu.

Hii inamaanisha kuwa uchambuzi wetu unakubaliana na mawazo ya Kunene pamoja na Senkoro kuwa safari ya shujaa siyo lazima ihusishwe na mwenendo wa kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine. Aidha, mtunzi katika kusawiri safari ya mhusika, anaweza kusawiri safari inayofanyika akilini mwa msomaji au msikilizaji bila mhusika kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Safari hii pia inaweza kuwa kwa kubadilisha umbo la mhusika (kumwua mhusika) na kumrejesha katika umbo lake tena. Jambo hili pia limejitokeza kwenye uchambuzi wetu ingawa siyo kwa kiwango kikubwa.

Katika ngano iitwayo *Mkono wa Birika Haufai,* fanani anatuambia kuhusu shujaa Buibui aliyepewa zawadi kutoka kwa mfalme. Buibui kutokana na uchoyo wake, alisafiri kutoka kijijini kwake ili aende mbali na kupika chakula alichopewa na mfalme mwenyewe kwani hakutaka hata nzi kunusa chakula chake. Buibui alipofika msituni ambapo alidhani hakuna watu, alipika chakula chake lakini kwa bahati mbaya, kulitokea Jini aliyemtaka Buibui amlishe chakula chake chote. Buibui alipokataa kumlisha jini chakula, jini alimuua Buibui. Fanani anasema:

> Buibui akamwambia, nimesema siendi pale. Walizozana sana kisha Jini alimroga Buibui kwa kusema "*Ayiyiteku*" hapo Buibui alikufa na Jini alibaki pale pale tangu siku ile. Kwa kadiri Jini alivyozidi kukaa pale kwa muda, alimrudisha Buibui uhai kwa kusema "Ayiyi tegborgbe" halafu Buibui alirudi tena hai.

Nukuu hapo juu inatuonesha kuwa kulikuwa na safari isiyohusishwa na mwenendo wa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Mhusika anabadilishwa kutoka katika hali yake ya kawaida na kupelekwa katika hali nyingine na kurudishwa tena. Tunaona jambo hili kama safari isiyowezekana kwa mwendendo wa kutoka sehemu moja kwenda nyingine bali safari ya ndani au ya kubadilisha umbo moja kwenda lingine.

Katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, mwandishi Shaaban Robert anaonesha usawiri wa ruwaza ya shujaa kwa njia ya safari ya kubadilisha umbo kupitia ndugu zake Adili. Mwandishi anatuambia kwamba kutokana na tendo la ndugu zake Adili la kumtosa Adili kwenye bahari ili afe, kwa tamaa ya kumpata msichana ambaye Adili alimleta mwenyewe, rafiki yake Huria aliwalaani ndugu zake Adili na wakageuka manyani. Mwandishi anasema:

> Kwa sababu hiyo walikuwa hatarini milele. Walakini alikubali kuwasamehe kwa sharti ya kuwageuza wanyama. Aliwalaani watoke katika umbo la uanadamu.Mara ile ndugu zake walikuwa manyani (uk. 40).

Dondoo hili linaonesha kuwa Shaaban Robert hatofautiani na jamii ya Waewe katika kusawiri ruwaza ya shujaa. Katika kazi zote mbili ruwaza ya shujaa imejengwa juu ya msingi wa motifu ya safari ya msako, na pia juu ya safari zinazofanyika katika mawazo ya wahusika, hadhira au wasomaji. Pamoja na kufanana huku, Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa pia inatambua kuwa kila jamii ina namna yake ya kuelezea ruwaza ya shujaa. Ili kulitekeleza jambo hili, mwandishi amefafanua jinsi jamii ya Waewe inavyotofautiana na jamii ya Watanzania kupitia ngano na riwaya zilizochambuliwa.

## 4.2 Utofauti wa Ujitokezaji wa Ruwaza ya Shujaa katika Matini Teule

Vigezo vilivyotumika kufafanua tofauti hizi vimetokana na nadharía iliyopendekezwa katika utangulizi wa makala haya. Hivyo, tumezingatia ruwaza za kuondoka, ruwaza ya majaribu, na ruwaza ya kurejea kwa wahusika. Kadhalika, tumezingatia usawiri wa ruwaza ya shujaa kupitia motifu ya safari isiyoonekana waziwazi.

### 6.2.1 Utofauti katika Kuondoka kwa Shujaa

Kwa kawaida, shujaa huondoka nyumbani kwao na kwenda kuishi katika nchi au sehemu za mbali na nyumbani. Sababu kuu mojawapo ya shujaa kutoka nyumbani kwao hutokana na tishio la maangamizo la maadui zake. Maadui zake ambao zaidi ni wafalme au viongozi, huhofia kuwa huenda shujaa ambaye huwa na uwezo mkubwa kuliko wao akawavamia wakati wowote na kufanya mapinduzi katika dola zao na kisha kutamalaki. Mungaigichamba (2005) anasema, safari ya shujaa kutoka nyumbani kwao ni muhimu sana kwani humtayarisha shujaa kutekeleza jukumu au dhima yake katika jamii. Jambo hili limejitokeza tofautitofauti kati ya fasihi simulizi ya Waewe na katika fasihi andishi ya Waswahili.

Katika ngano za Kiewe shujaa anakimbia kutoka kwao kwa sababu ya njama ya kuuawa. Kwa mfano, katika ngano iitwayo *Umoja ni Nguvu* safari waliyofanya Farasi, Jogoo, Paka na Kuku wote kutoka sehemu mbalimbali. Mashujaa hawa walikuwa wanaihudumia jamii yao kwa namna mbalimbali lakini ilifika wakati ambapo jamii ilitaka kuwaua, kwa hiyo, walikimbia kutoka kwao kuelekea sehemu yenye amani zaidi ili wasife nyumbani. Kwa mfano fanani anasema:

> Farasi alisikia kila kitu na hivyo akaamua kutoroka alfajiri na kwenda sehemu ya mbali ili afe kifo cha kawaida kuliko kuuwawa na mtu.

Hivyo, kinachobainika hapa ni kuwa shujaa aliondoka kutokana na njama ya kutaka kuuawa. Hata hivyo, suala hili linasawiriwa kwa namna tofauti kidogo katika riwaya teule. Katika riwaya teule, mashujaa wanaondoka kwenda safarini kwa utashi au hamu zao. Kwa mfano, katika *Kusadikika* wajumbe wote waliondoka mmoja baada ya mwingine kwa kutaka wenyewe bila mtu yeyote kuwazuia. Wajumbe hao wote waliondoka kwa ridhaa yao na walisafiri kwenda nchi za mbali ili wajifunze namna bora za kuleta maendeleo katika nchi yao. Kwa hiyo, utofauti unaojitokeza hapa baina ya ngano na riwaya ni kwamba katika ngano za Kiewe, shujaa anaondoka ili aepuke kuuawa na watu wake lakini katika *Kusadikika* shujaa anaondoka ili alete mbinu za maendeleo katika jamii yake.

### 4.2.2 Utofauti katika Shujaa Kukutana na Majaribu

Kwa kawaida, shujaa hakosi maadui au upinzani. Hali hii pia hujitokeza katika maisha ya kawaida ambapo ingawa mtu fulani ni mashuhuri au ana ufanisi mkubwa, hapakosi maadui kadhaa ambao humwonea kijicho na kumtakia maovu na hata kujaribu kumwangamiza. Katika ngano za Kiewe, siyo kila wakati shujaa anavishinda vikwazo. Kwa vile, ngano mara nyingi husimuliwa ili kukosoa tabia fulani au kuelimisha jamii na kadhalika, hadithi haiwezi kuhimiza tabia mbaya ya shujaa kama anayo kabla hajaondoka nyumbani.

Katika hadithi ya *Asiyesikia la Mkuu, Huvunjika Guu* fanani anatuambia kuhusu tabia ya Atsu aliyekataa ushauri wa wazazi wake kutokwenda shambani usiku kutafuta filimbi yake. Ingawa Atsu aliweza kushinda vikwazo vingi ikiwa ni pamoja na giza nene, misitu mikubwa na mirefu, sauti za kutisha na mengine, lakini alipopata filimbi na kuanza kuimba kwa furaha huku akicheza, anavamiwa na wanyama wakali na kuuawa. Kupitia hadithi hii, tunatambua kuwa siyo kila mara wahusika au mashujaa wanaosawiriwa kwenye ngano za Kiewe wanashinda. Kuna wakati mashujaa hao wanashindwa. Ingawa anguko au kifo cha shujaa wakati mwingine kinasikitisha sana, pia kinatumika kutoa ujumbe maalumu kwa wanajamii katika kujitoa mhanga. Kwa upande mwingine mashujaa wanaoshindwa vitani kutokana na jitihada zao kuokoa jamii yao wanaenziwa na jamii.

Kwa upande mwingine, hali iko tofauti katika riwaya ya *Kusadikika*. Hii ni kwa sababu kila mara mashujaa/wahusika walipokutana na vikwazo walivishinda. Katika riwaya ya *Kusadikika*, tunamuona kila mjumbe akishinda vikwazo anavyokutana navyo katika safari yake. Kwa mfano, mjumbe wa Kaskazini alipewa jukumu la kusafiri, kutalii na kuandika habari za mambo ya nchi ngeni aliyofikiri kwamba yangeiletea Kusadikika ustawi. Shujaa huyu, alikutana na vizuizi vingi lakini mwandishi anasema: "Kila alipokutana na shida ndipo bidii yake ilipozidi kukua" (uk. 11).

Vilevile, wajumbe wengine wote walipitia vikwazo vingi katika safari zao lakini kila mtu alishinda vikwazo hivi na kurudi nyumbani salama. Hii inamaaisha kuwa katika jamii ya Waewe shujaa anaweza kuzidiwa na hali au mazingira na hatima yake ushujaa wake usionekane kupitia kushinda. Hata hivyo, hali hiyo haina maana kuwa yeye siye shujaa. Hii ni tofauti katika riwaya ya *Kusadikika* ambapo tunaona kuwa mashujaa wote walishinda vikwazo safarini.

Jambo hili linajitokeza pia katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Japokuwa Adili alikutana na majaribu kadha wa kadha lakini aliyashinda. Adili anavishinda vikwazo kupitia msaada anaoupata kutoka kwa Huria. Hii ni tofauti na ngano ya *Asiyesikia la Mkuu Huvunjika Guu,* ambapo shujaa Atsu hakushinda vikwazo. Adili katika riwaya ya *Adili na Nduguze* alishinda vikwazo vya kutaka kuuliwa alipotoswa baharini.

### 4.2.3 Utofauti katika Kurudi kwa Shujaa

Nyamsenda (2015) katika utafiti wake kuhusu ushujaa katika jamii ya Waikizu nchini Tanzania anaeleza kwamba mara nyingi ushujaa wa Waikizu huwa ni kwa mustakabali wa jamii nzima ya Ikizu, ni lazima shujaa arudi nyumbani, na kama shujaa hatarudi nyumbani huyo kwao si shujaa. Kitendo cha shujaa kutorudi nyumbani tafsiri yake ni kwamba ameacha asili. Wazo la Nyamsenda linadhirika kwenye riwaya teule za Shaaban Robert tofauti na ilivyo katika ngano za Kiewe. Katika jamii ya Waewe, shujaa anasafiri kwa sababu mbalimbali, hata hivyo sio lazima arudi nyumbani. Kwa maneno mengine mhusika/shujaa asiporudi nyumbani, haimaanishi kuwa yeye sio shujaa. Kwa mfano kuna baadhi ya ngano ambapo tunasimuliwa kuwa shujaa ameondoka ili ajitafutie amani na furaha mbali na nyumbani kwake. Katika ngano ya *Kuwornu na Watoto zake* Mawusi aliamua kutoka nyumbani na kumwacha kaka yake na mke wake pekee yao. Mawusi alienda kukaa na kujijengea nyumba katika kijiji cha mbali. Katika kijiji

hicho, Mawusi alikuwa anaheshimiwa na kuchukuliwa na watu ya kijijini kule kama malkia wao. Katika hadithi hii, japokuwa Mawusi hakurudi, alionesha sifa zote anazokuwa nazo shujaa.

Pia katika ngano ya *Umoja ni Nguvu* pamoja na *Asiyesikia la mkuu huvunjika guu,* tunawaona mashujaa wakisafiri kwenda nchi za mbali sana na kutorudi nyumbani kwao walipoanzia safari. Hii ni tofauti na riwaya teule zilizochambuliwa kwenye makala haya. . Shaaban Robert anathibitisha katika riwaya zake kuwa shujaa lazima arudi, na asiporudi kwenye asili yake, basi yeye sio shujaa. Pamoja na kukataa wazo hili, tunaona kuwa safari ya msako haihusishi tu matembezi kutoka sehemu moja na kurudi sehemu hiyo hiyo. Aina nyingine ya safari ni safari ya makuzi ya maisha. Katika safari hii, shujaa akitoka kwenye hatua ya kwanza ya utoto, makuzi yake huendelea mpaka kifo chake. Kwa hiyo sio lazima shujaa arejee nyumbani kama Shabaan Robert na wengine wanavyofikiri.

### 4.2.4 Utofauti katika Usawiri wa Shujaa Mwanamke

Wasanii wengi kama kawaida huwasawiri wanaume kuwa ndio wanaoweza kila kitu. Mwanamke hupewa dhima ya umama, kuzaa, kuolewa, na kulea familia, na mambo yote mengine hupewa mhusika mwanamume. Sifa hizo hazikutazamwa kama sifa za ushujaa. Kinyume na hayo katika ngano zetu, mwanamke naye amepewa dhima ya kuwa shujaa. Zipo hadithi zilizomsawiri mwanamke kama shujaa. Maoni yetu yanajitokeza katika wazo la Mbele (2006) akionesha nafasi ya wanawake katika tendi za Kiafrika. Mtaalamu huyu anasema kuwa wanawake wana mchango mkubwa katika tendi za Kiafrika hasa katika dhana ya ushujaa. Hata hivyo, wasomi wengi wameshindwa kuonesha na kutambua ushujaa wao, badala yake wameweka msisitizo na kumtazama zaidi shujaa mwanamume kwa jicho pevu na kumsahau mwanamke na kufanya dhana ya ushujaa kuonekana katika mtazamo dume. Hivyo, Mbele anaona kuna haja ya kuangalia dhana ya ushujaa wa mwanamke kwa kuchunguza sanaa jadi. Mtazamo wa Mbele ni kuwa tendi zina uhusiano mkubwa na tanzu nyinginezo hususani ngano.

Kupitia uchambuzi wa ngano za Kiewe, makala haya yamegundua kuwa suala la ushujaa linawahusu wanawake na wanaume. Aidha, Raglan (1979) ameonesha ushujaa wa mashujaa wanawake na kutaja sifa za mashujaa hao ambazo zinafanana na sifa za mashujaa wanaume. Tunaunga mkono mwazo ya wataalamu hawa kwa kuwa hata katika ngano tulizochambua jambo hili limedhihirika. Kwa mfano, katika hadithi ya *Asiyesikia la Mkuu Huvunjika Guu,* tunasimuliwa kuhusu watoto pacha

Atsu na Atsupui. Atsupui ni msichana ambaye baada ya kuuawa kwa kaka yake na wanyama porini, alifunga safari ya kwenda kumtafuta kaka yake. Japokuwa kwa umri wake ni hatari kwenda peke yake msituni lakini alienda safari hiyo bila woga. Baada ya kugundua kwamba kaka yake kweli aliuawa na wanyama, alirudi na kwenda kwa mfalme na wazee wa kijiji chake ili kuwataarifu kuhusu kifo cha kaka yake. Ujasiri aliounesha Atsupui ni wa pekee kabisa.

Kadhalika, katika hadithi ya *Asana na Fuseini,* fanani anamsawiri mwanamke kama shujaa kwa kumwokoa kaka yake. Katika hadithi hii, tunasimuliwa kuwa Asana ambaye ni msichana mwenye umri mdogo alienda kuvua samaki pamoja na kaka yake ili waweze kupata chakula kwa vile wazazi wao walifariki. Wakati wa kuvua samaki, siku moja kuna Chunusi kubwa aliyemkamata Fuseini na kuondoka naye. Asana naye alifunga safari yake kuingia kwenye maji na kupambana na Chunusi mpaka alimshinda na kumwokoa kaka yake. Fanani anathibitisha hili kwa kusema:

> Siku moja Asana aliamua kuzamia kwenye maji na kumtafuta kaka yake. Alizamia chini zaidi ingawa alipata shida kupumua, … Asana alikwenda na kupambana naye mpaka akamzidi Chunusi na kumua, kisha akamuokoa kaka yake akiwa bado hai.

Mwandishi wa makala haya anaona kuwa kujitokeza kwa shujaa mwanamke katika ngano za Kiewe kunaonesha tofauti kati ya ruwaza ya shujaa anayesawiriwa kwenye ngano na yule anayesawiriwa kwenye riwaya teule. Katika riwaya zake, Shaaban Robert alionesha nafasi ya mwanamke kama mhusika aliyemsaidia shujaa kunusuru kifo na kushinda vikwazo (rej. *Adili na Nduguze*). Hivyo, katika riwaya za Shaaan Robert mwanamke amesawiriwa kama mhusika anayemsaidia shujaa kutimiza malengo yake. Kwa mujibu wa Mungaigichamba (2005), mwanamke anaweza kutenda tendo moja la ujasiri lakini tendo hili halimpi kibali cha kuwa shujaa. Ujasiri ni sifa mojawapo tu ya mashujaa. Sifa hii pia hupatikana hata kwa wanadamu wengine wa kawaida ambao huwa hawachukuliwi kuwa mashujaa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Adili na Nduguze,* Huria amechorwa kama ni jasiri pale alipojitosa baharini kumuokoa Adili.

Hivyo, kutokana na maelezo haya, ujasiri wa Huria na msaada wake aliouonesha vinaweza kuchukuliwa kama sifa za kiushujaa lakini Huria mwenyewe siyo

shujaa kama ilivyo katika ngano za Kiewe ambapo tumesimuliwa kuhusu safari za mashujaa hao. Hii haimaanishi kuwa hakuna shujaa mwanamke katika jamii ya mwandishi Shaaban Robert. Inawezekana kutokana na mtindo aliokusudia kuutumia, hakutaka kumpa mwanamke fursa kamili ya kujitokeza kama shujaa kama walivyo wanaume ila wanatoa mchango mkubwa kwa shujaa wa kiume.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yalikusudia kuchambua ngano za Kiewe na riwaya teule za Shaaban Robert ili kuonesha ujitokezaji wa ruwaza ya shujaa. Jambo hilo limekabiliwa kwa kutumia misingi maalumu ya Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa. Matokeo ya uchambuzi wa data yanaonesha kuwa kuna mfanano na utofauti katika namna ya kusawiri ruwaza ya shujaa. Katika kazi zote zilizochambuliwa, ruwaza ya shujaa imedhihirishwa kupitia nyenzo kuu tatu za kisanaa: dhana ya ushujaa, sifa za shujaa, motifu ya safari, msako na motifu ya safari ya msako. Kwa nyenzo hizo, Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa imeonekana kuwa faafu katika kuyakabili masuala yanayohusu shujaa na usawiri wake. Pia, kuna mfanano mkubwa katika jinsi fanani wa ngano za Kiewe wanavyomsawiri shujaa ikilinganishwa na jinsi mwandishi Shaaban Robert alivyomsawiri shujaa huyo. Makala haya pia yamepambanua tofauti mbalimbali zinazojitokeza katika usawiri wa ruwaza ya shujaa katika kazi za kifasihi zilizochambuliwa. Mwandishi anahitimisha kuwa fasihi ni msingi imara na thabiti unaoweza kuonesha uhusiano uliopo kati ya jamii moja na nyingine. Uchambuzi wetu umedhihirisha kwamba kwa namna ya kipekee jamii ya Waewe na jamii ya Waswahili zinahusiana mno kifasihi. Tafiti zaidi zinahitajika ili kuonesha sababu hasa zinazochochea kushabihiana na kusigana kwa baadhi ya masuala yaliyojadiliwa ndani ya makala haya.

## Marejeleo

Campbell, J. (1973). *The Hero with a Thousand Faces.* Princeton: Bolingeu.

Dzakpasu, T. E. (1981). "Gli An Ewe Performance Art." Master of Arts, University of Ghana, Legon (Haijachapishwa).

Kiango, S. D. (1974). *Utafiti wa Amali za Fasihi Simulizi.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Kunene, D. P. (1985). "*Journey as Metaphor in Africa Literature*" *Stephen A. Mh. African Literature Studies:* The Present State/L' et al., Present. Washington: Three Continents Press.

Matteru, B.N. (1983). "Fasihi Simulizi," Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Fasihi*. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam: TUKI.

Mbele, J. L. (2006). Women in the African Epic, Research in African Literatures, 37 no 2. 61-67; British Library Serials.

Mwai, W. na Ndungo, W. (1991). *Kiswahili Studies: Part Two*. Nairobi: University of Nairobi.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Huria.

Mulokozi, M. M. (Mhariri) (1999). *Tenzi Tatu za Kale.* Dar es Salaam: TUKI.

Mungaigichamba, J. (2005). "Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao Kwa Jamii zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu". Tasnifu ya Umahiri ( Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi

Ndugo C.M. na Wafula R.M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008) Chapa ya Pili. *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Nkwera, F. (1979). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Nukunya, G.K. (1992). *Tradition and Change in Ghana: An Introduction to Sociology.* Accra: Ghana University Press.

Nyamsenda, J.C. (2015). "Ushujaa Wa Shujaa wa Motifu Za Safari na Msako Katika Ngano za Waikizu, Wabondei Na Wazanzibari". Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature Background, Character and Continuity.* Bloomington and Indianapolis: Indiana University Press.

Propp, V. (1958). *Morphology of Folktale*. Bloomington: Indiana University Press.

Raglan, L. (1979). *The Hero.* New York: Median.

Robert, S. (1991). *Kusadikika.* Nairobi: Nelson Nairobi.

Robert, S. (2010). *Adili na Nduguze,* Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Saleh, K.K. (2015). "Ufasihi Simulizi Katika Riwaya za Shaaban Robert: Mifano Kutoka *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*". Tasinifu ya Umahiri ( Haijachapishwa) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi.* Dar es Salaam: MEVELI Publishers.

Senkoro, F. M. K. (1997). "The Significance of the Journey in FolkTales from Zanzibar." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sidahome, J.E. (1964). *The Stories of The Benin Empire*. Ibadan: Oxford University Press.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford Universty Press.

TUMI (1988). *Kiswahili Sekondari.* Dar es Salaam:TUMI.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi: English Press.

Whorf, B.L. (1956). "Language, Mind and Reality" Carrol, J.B Mh. (1972) Language, Thought and Reality. MIT Press: Imechukuliwa kutoka The Conch, 4.